



Mtume Sallalaahu `Alalihi Wasallam amesema: **“Yeyote anayezua au akampokea vizuri mzushi (mtu wa bid’ah) basi juu yake laana ya Allah, malaika Wake, na ummah mzima”** [Imepokewa na Bukhari (12/41) na Muslim (9/140)]

Ibn Umar (radhiallaahu `anhu) amesema: “Kila jambo la uzushi ni upotofu, hata kama watu wataliona kuwa ni jambo zuri.” [Imepokewa na Abu Shaamah na. 39]

Ibn `Abbaas (radhiallahu anhumaa) amesema: “Kwa hakika jambo la kuchukiza zaidi mbele ya Allah ni mambo ya uzushi” [Imepokewa na al-Bayhaqee katika as-Sunan al-Kubraa (4/316)]

Sufyaan ath-Thawree (rahimahullah) amesema: “Mambo ya uzushi yanampendeza zaidi Shetani kuliko dhambi, kwani mtu hutubia kutokana na madhambi yake walakin hatubii kwa mambo ya uzushi.” [Imepokewa na al-Laalikaa’ee katika Sharh Usool I’tiqaad Ahlis-Sunnah wal-Jamaa’ah (no. 238)]

Abu Haatim (rahimahullah) amesema: “Alama ya watu wa bid’ah ni kule kupingana kwao na watu wa upokezi wa riwaya.” [Imepokewa na al-Laalikaa’ee katika Sharh Usool I’tiqaad Ahlis-Sunnah wal-Jamaa’ah Volume 1, uk. 179]

Sufyaan ath-Thawree (rahimahullah) amesema: “Yeyote anayemsikiliza mzushi basi atakuwa ameondoka katika hifadhi ya Allaah na amejiunga na mambo ya uzushi.” [Imepokewa na Abu Nu’aym katika al-Hilyah (7/26) na Ibn Battah (na. 444)]

Ibraheem ibn Maysarah (rahimahullah) amesema: “Yeyote anayemtukuza mzushi basi atakuwa amesaidia katika kuuangamiza Uislamu” [Imepokewa na al-Laalikaa’ee katika Sharh Usool I’tiqaad Ahlis-Sunnah wal-Jamaa’ah (no.1/139)]

Al-Awzaa’ee (rahimahullah) amesema kuwa: `Umar ibn `Abdul-`Azeez (rahimahullah) amesema: “Mutakapo ona watu wakikutana kisiri kuhusu mambo ya dini juu ya jambo lolote pasi na kuwahusisha watu wa kawaida – basi jueni yakwaba hao wako katika misingi ya upotofu” [Imepokewa na al-

Misemo Ya Salaf as-Saalih Kuhusu Bid'ah na Watu Wake.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Laalikaa'ee katika Sharh Usool I'tiqaad Ahlis-Sunnah wal-Jamaa'ah (no. 251)]

Al-Hasan al-Basree (rahimahullaah) amesema: Musishiriki katika vikao vya watu wa bida'h (uzushi) na (watu) wenye kufuata matamano yao, wala musibishane nao, wala musiwasilize. [Imepokewa katika Sunan ad-Daarimee (1/121)]

Al-Fudayl bin 'Iyaad (rahimahullaah) amesema: Nilikutana na watu walio bora, wote walikuwa ni watu walioshikamana na sunnah na walikuwa wakikataza kuandamana na watu wa bida'h. " [Imepokewa na al-Laalikaa'ee katika Sharh Usool I'tiqaad Ahlis-Sunnah wal-Jamaa'ah (na. 267)]

Imaam Abu Haneefah (rahimahullah) amesema: "Shikamana na hadeeth na njia ya Salaf as-Saalih (watangulizi wema), na jihadhari na mambo mapya yanayozuliwa, kwani yote hayo ni bid'ah." [Imepokewa na as-Suyutee katika Sawnul Muntaq uk. 32]

Imaam Malik (rahimahullah) amesema: "Yeyote anaeanzisha katika Uislamu jambo la uzushi, na akalidhania kuwa ni zuri, basi huyo amedai yakwamba Mtume Muhammad (Sallallahu Alaihi Wasallam) amefanya khiyana katika (amana ya kuufikiliza) ujumbe."

Amesema tena: "Uovu ulioje walionao watu wazushi, hatuwapi hata salaam!" [Imepokewa na al-Baghawee katika Sharh us-Sunnah na. (1/234)]

Imaam ash-Shaafi'ee (rahimahullah) amesema: "Mtu akutane na Allaah awe amefanya kila aina ya dhambi isipokuwa Shirki tu, ni bora kuliko kukutana na Allaah na ibadah yoyote katika bid'ah." [Imepokewa na al-Bayhaqee katika al-I'tiqaad (uk.158)]

Al-Layth bin Sa'd (rahimahullah) amesema: "Hata kama lau ningelimuona mtu wa hawaa (matamaniwa – yaani mtu wa bid'ah) atembea juu ya maji, nisingelikubali" Basi Imaam ash-Shaafi'ee (rahimahullah) nae akasema: "Yeye (al-Layth) ameteleza kidogo (katika maneno yake). Mimi hata kama ningelimuona atembea angani, nisingelikubali chochote kutoka kwake. [Imepokewa na as-Suyooti katika al-Amr bil 'Ittibaa wan-Nahee anil Ibtidaa']

Imaam Ahmad (rahimahullah) amesema: "Katika nguzo muhimu za sunnah kwetu sisi ni: kujiepusha na mambo ya kuzua na kila jambo la uzushi ni upotofu." [Katika kitabu chake Usool as-Sunnah uk. 1]